**TANGAZO LA ZABUNI**

**SHDEPHA+ NETWORK FOR PLHA, KAHAMA BRANCH, P.O BOX 564, KAHAMA, TEL: 028-2710730, MOB: +255 785 820 330** Email: shdephakahama@yahoo.com

TANGAZO LA TENDA YA KUSHONA SARE ZA SHULE KWA WANAFUNZI WA SHULE ZA MSINGI.

**UTANGULIZI**

SHDEPHA+ Ni Shirika lisilo la kiserikali, Limesajiliwa Tarehe 21/11/1994 kwa Nambari ya Usajili 8216. Shdepha + Ina matawi zaidi ya 5 kote nchini.shirika la SHDEPHA + Limekuwa Likifanya Kazi na Wahisani Wote wa Kitaifa na kimataifa , Serikali kuu na serikali za Mitaa, na Wadau mbali mbali katika utekelezaji wa Shughuli zake za kuihudumia jamii kupitia miradi mbali mbali ya kiafya ikiwemo UKIMWI,KIFUA KIKUU,MALARIA, ELIMU na miradi inayohusiana na maswala mazima ya UJINSIA .

SHDEPHA + kwa kushirikiana na Pact-Tanzania inatekeleza Mradi wa USAID ACHIEVE katika Halmashauri za Msalala, Kahama mji na Ushetu.Kupitia Mradi huu, SHDEPHA + imepanga kutoa ufadhili wa Sare za Shule kwa wanafunzi 411 wa shule za Msingi kutoka kaya zenye mazingira magumu. Lengo la ufadhili huu nikuongeza Morali ya wanafunzi lengwa kuhudhuria shule, kujifunza kikamilifu nakupunguza utoro unaosababishwa na kukosa sare. Ni imani yetu kuwa endapo wanafunzi hawa watapatiwa sare siyo TU morali ya kuhudhuria shule itaongezeka ila pia ufanisi wao katika masomo utaongezeka maradufu.
Kwa Mantiki hiyo, SHDEPHA + inapenda kuwatangazia watu wote wenye sifa na uwezo; binafsi, Vikundi au Makampuni wanaojishughulisha na kazi za kushona na kusambaza sare za Shule ndani ya wilaya ya Masasi kutuma Maombi ya tenda ili kutimiza lengo hilo la kuwapatia wanafunzi Sare.

***Maelekezo***: *Fomu hii inaelezea sifa za sare kwa wanafunzi wa shule za msingi wa kike/ kiume ambao ni wanufaika wa mradi wa ACHIEVE, unaofadhiliwa na watu wa Marekani (USAID).*

**Sifa za Sare za shule**

| **Na** | **Bidhaa** | **Sifa** |
|---|---|---|
| 1 | Shati | Shati jeupe (Tomato) lenye mfuko mmoja upande wa kushoto |

| | | |
|---|---|---|
| 2 | Sketi/gauni | Sketi/gauni za watoto wa kike kulingana na rangi za shule husika. |
| 3 | Kaptula/Suruali | Kaptula au Suruali za watoto wa kiume kulingana na rangi za shule husika |
| 4 | Soksi | Soksi kulingana na rangi za shule husika |
| 5 | Sweta | Lililofumwa kwa nyuzi kulingana na rangi za shule husika. |

*Aina, saizi na rangi lazima zihakikiwe na mzabuni kulingana na uhalisi wa shule husika.

*Mzabuni anatakiwa aombe zabuni ya manunuzi ya unifomu kwa ajili ya watoto kuanzia watoto **100** (ambazo itakuwa na sketi/gauni (**moja**) au Kaptula/suruali (**moja**)-, Shati (**moja**-aina Tomato), soksi **(jozi 2)** na Sweta la shule (**moja**).

**Mzabuni anatakiwa awe na vitu vifuatavyo:**

- Risiti ya mashine (EFD).
- Uwezo wa kukabidhi sare kama mkataba unavyoonyesha pasipo kupewa malipo ya awali.
- Awe mkazi wa wilaya/kata wanapotoka walengwa wa mradi.
- Awe na uwezo wa kufika katika kata husika kuchukua vipimo vya wanafunzi na kuona aina na rangi ya sare.
- Awe na uwezo wa kuambatanisha sampuli ya bidhaa (shati, soksi, kitambaa cha sketi/gauni/kaptula/suruali, sweta) pamoja na maombi yake ya zabuni.
- Fomu ya maombi ya zabuni lazima igongwe mhuri/dole gumba.

Kwa wote watakaohitaji, tafadhali fika ofisi ya Asasi (LIP) ya wilaya iliyopo Kahama kwa ajili ya kuchukua fomu za maombi ya zabuni kuanzia tarehe 13/6/2022 hadi 26/6/2022.

Wazabuni watatakiwa kuona sampuli ya sare za shule watakapoenda kwenye ofisi ya Asasi (LIP) kuchukua fomu ya maombi ili kujua rangi na aina ya sare kabla ya kuomba zabuni. Ifahamike kwamba mzabuni atatakiwa kutengeneza sare za shule kulingana na sampuli atakayoleta mtoto siku ya upimaji wa sare, hivyo sampuli inayoonyeshwa na Asasi ni kuwapa picha ya karibu ili waweze kuomba zabuni.

Wazabuni watakaotuma maombi wanatakiwa kuwasilisha ofisi ya Asasi (LIP) ya wilaya vitu vifuatavyo vikiambatana na fomu zao za maombi ya zabuni:

1) Nakala ya leseni ya biashara, Namba ya usajili wa biashara (TIN)
2) Nakala ya kitambulisho cha taifa (NIDA)
3) Muda atakaotumia kuleta sare shuleni.

Wazabuni watakaohitaji wawasilishe maombi yao kwa:

**Mkurugenzi wa Asasi**

**Ofisi ya Asasi: SHDEPHA + KAHAMA**

**Wilaya: KAHAMA.**

Maombi yote yawasilishwe katika bahasha iliyofungwa. Mwisho wa kupokea maombi ni 26/6/2022 Saa kumi na moja jioni.

**Tafadhali kumbuka**:

1. Maombi kwa njia ya barua pepe au simu hayatapokelewa.
2. Asasi inaweza kumkataa mzabuni atakayegundulika kupitishwa pasipo kukidhi vigezo.
3. Asasi wanaweza kukataa ombi lolote au maombi yote yaliyopokelewa.
4. Asasi ina haki ya kuyakataa maombi yoyote yatakayowasilishwa na mzabuni pasipo kufuta taratibu zilizowekwa.
5. Asasi ina haki ya kuruhusu kufanyika kwa marekebisho kwa makosa madogo kwa waombaji wa zabuni ili kuongeza nafasi ya ushindani.
6. Asasi watawasiliana na wazabuni wote waliotuma maombi ili kuwahakiki waombaji pamoja na anuani zao.
7. Malipo yatafanyika kupitia asasi ya kijamii.

SHDEPHA+ INAFANYA KAZI KWA KUZINGATIA MISINGI MBALIMBALI IKIWEMO HAKI ZA WATOTO,KUPINGA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU NA KUWAKUZINGATIA MAADILI YA SHIRIKA ,HIVYO WAZABUNI WOTE WATAKOVUTIWA NA ZABUNI HII WATATAKIWA KUFUATA MISINGI YASHIRIKA KAMA ILIVYOAINISHWA HAPO CHINI.

- Kukubali kufanyiwa ukaguzi wa kutokuwekewa masharti yakufanya kazi na USAID ( Supplier vetting)
- Kutojihusisha kwa namna yoyote na biashara haramu ya usafirishaji binadamu( Anti trafficking)
- Kutojihusisha na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa namna yoyote –hii hujumuisha wafanyakazi wote kwa mzabuni atakayechaguliwa.
- Kutojihusisha naukiukaji sheria zinazomlinda mtoto(chini ya miaka 18)

Kwakuzingatia hili mzabuni/wazabuni watakao chaguliwa watatakiwa kudhibitisha uelewa nakutojihusisha na mambo hayo yaliyoainishwa hapo juu.
Tarehe za mchakoto huu wa zabuni

| Maelezo | Tarehe |
|---|---|
| Mwaliko wa zabuni | 13/6/2022 |
| Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha maombi | 26/6/2022 |
| Ufunguzi wa zabuni | 27/6/2022 |
| Kamati ya mapitio ya zabuni | 27/6/2022 |
| Ukaguzi, tathmin na majadiliano | 28/6/2022 |
| Kutoa zabuni | 28/06/2022 |